MWANGA WA LUGHA



Jarida la Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Moi

Juzuu 3 Na.1

Aprili 2019

DR C. NYANDIBA
22/07/2019

Mwanga wa Lugha

Mwanga wa Lugha

MOI UNIVERSITY
PRESS

Moi University Press, Moi University, Eldoret

© Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,
Chuo Kikuu cha Moi

Kimechapishwa 2019

Chapa ya Kwanza 2019

ISSN 2412-6993

Kimetoleshwa na:
Utafiti Foundation
Pioneer Estate, Off Kapsabet Road,
P. O. Box 884 – 30100, Eldoret, Kenya.
Tel: +254-053-206-302-4
Website: www.utafitifoundation.com

Yaliyomo

Mchango wa Wanawake wa Kiswahili katika Uongozi, Dini na Ushairi 1350 B.K-1840 B.K.
Kineene wa Mutiso.....1

Matumizi ya Kiswahili katika Kuhamasisha Umma kuhusu Afya: Mtazamo wa Mawasiliano
Jacktone Okello Onyango.....27

Matumizi ya Vielelezo vya Kihisabati katika Fafanuzi za Fahiwa Mbalimbali
Benard Okal.....41

Uchanganuzi wa Muziki Uliopendwa na Muziki wa Kisasa
Carren Nyandiba.....63

Tafsiri Tenge katika Matini Zilizotafsiriwa kwa Tafsiri-Mashine: Uchanganuzi wa Matini za Kiingereza-Kiswahili
Sarah Ngesu.....75

Towards an Authentic African Literary Tradition: Ngũgĩ Wa Thiong'o's Rewriting of *The Pilgrim's Progress* in *Devil on the Cross*
Nicholas Kamau-Goro.....93

Language Use amongst Multilingual Learners and their Teachers in a Pre-School Classroom in Nakuru County, Kenya
Mary Mubia, Felicia Yieke and *Evelyn Mahero*.....105

Kiswahili kama Lugha Changizi: Uchambuzi wa Kifonolojia wa Maneno Yaliyokopeshwa Lugha ya Kikikuyu
P. I. Iribemwangi.....125

Nafasi ya Kiswahili katika Utoaji wa Huduma za Afya Tanzania
Adventina Buberwa.....147

Historically Grounded Symbolism and the Thematic Lacuna in Translation: The Translation of *Treasure Island* into Kiswahili as *Kisiwa Chenye Hazina*
James Omboga Zaja.....163

Uchanganuzi wa Muziki Uliopendwa na Muziki wa Kisasa

Carren Nyandiba
Chuo Kikuu cha Rongo

Ikisiri

Muziki ni mojawapo ya vipera muhimu vya fasihi simulizi. Jumbe muhimu kuhusu masuala mbalimbali yanayoathiri jamii huwasilishwa kupitia muziki. Aidha, muziki umeweza kutumika kutoa habari kuhusu mambo ambayo huchukuliwa mwiko na, kwa hivyo, hayawezi kujadiliwa katika vikao na mazungumzo ya kawaida. Baadhi ya sifa za muziki zinazoufanya kutumika kwa urahisi ni pamoja na matumizi ya tamathali za usemi (kama vile mafumbo, methali na tashbihi) midundo na matumizi ya mahadhi yanayotokana na ala zinazotumika katika muziki. Makala haya yananuia kulinganisha muziki uliopendwa na muziki wa kisasa. Ulinganishi utahusu matumizi ya mapambo ya lugha kama vile tamathali za usemi, methali, semi na mafumbo katika aina hizo mbili za muziki kwa lengo la kuonesha ni muziki upi ulio na matumizi pevu ya lugha na hivyo unaoweza kutumika katika kuendeleza lugha ya Kiswahili. Muziki wa bendi ya DDC Mlimani Park utatathminiwa kwa kuzingatia kategoria ya muziki uliopendwa na ule wa bendi ya Sauti Sol katika kategoria ya muziki wa kisasa.

Maneno Muhimu: Muziki, uliopendwa, kisasa, jamii

Utangulizi

Muziki ni sehemu muhimu ya jamii nyingi za ulimwengu. Aidha muziki hutumiwa na jamii katika kutekeleza majukumu na dhima mbalimbali. Muziki katika jamii una dhima ya kuelimisha, kutambulisha, kupitisha historia, kusambaza habari muhimu, kuonya na kuadilisha miongoni mwa dhima nyingine (Nyandiba, 2014; Ntarangwi, 2007). Nyimbo kama kipera cha fasihi simulizi huweza kutumika kama wenzo wa kuelimisha kwa njia anuwai. Kwa mfano, maudhui katika nyimbo yanaweza kutumika kama mbinu ya kupitisha elimu na maarifa kwa wasikilizaji wa nyimbo hizo. Pia, mtu anaweza kujifundisha vipengee mbalimbali vya lugha kupitia kwa muziki. Hii ni kwa sababu muziki, kama vile mashairi, hutungwa kwa lugha ya kipekee, yenye kuteka hisia za msomaji au msikilizaji.

Kuna aina mbalimbali za muziki. Kwa mfano, kuna muziki wa kiasili au kienyeji (Mindoti, 2014), muziki uliopendwa (Ngugi, 2000), muziki wa Kiafrika (Shitandi, 2014) na Muziki wa kisasa (Mulongo, 2012) miongoni mwa aina nyingine. Hata hivyo, lengo la makala haya si kufafaua aina za muziki, bali ni kueleza lugha inayotumika katika utunzi wa muziki. Kiini cha makala ni kulinganisha lugha iliyotumika katika utunzi wa muziki uliopendwa na muziki wa kisasa ili kuonesha ni muziki upi uliotumia lugha pevu zaidi na hivyo unaweza kutumika katika kufundisha Kiswahili. Makala haya yaandikwa kwa kuzingatia madai ya Mulongo (2012) kwamba wanafunzi wengi katika shule za upili hawapendi ushairi, hata hivyo, wanafunzi hao hao hupenda sana muziki wa kizazi kipya na kwamba muziki basi unaweza kutumika katika kufundishia. Kwa kuzingatia maoni hayo, makala yanalenga kuhoji iwapo mbali na kutumika kufundishia ushairi, muziki unaweza kutumika katika kufundisha vipengele vinginevyo vya lugha. Kwa vile tamathali za usemi ni kipengele cha lugha, makala haya yanadhamiria kuchanganua umwafaka wa kutumia nyimbo katika kufundishia kipengele hicho. Muziki utakaoangaziwa ni ule ujulikanao kama muziki uliopendwa na muziki wa kisasa. Baadhi ya maswali ambayo makala haya yanalenga kujibu ni pamoja na: Je, muziki uliopendwa ni upi na ule wa kisasa ni upi? Je, lugha iliyotumiwa katika utunzi wa aina hizo za miziki ipi? Kati ya muziki uliopendwa na muziki wa kisasa, ni upi ulio na matumizi pevu ya lugha?

Muziki Uliopendwa

Kwa mujibu wa Ngugi (2000), dhana ya nyimbo zilizopendwa ilianza kutumiwa zamani sana, kurejelea nyimbo zilizoimbwa na wasanii mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wasanii walioimba nyimbo zilizojulikana kama 'zilizopendwa' ni wale walioimba katika miaka ya sitini hadi sabini. Waimbaji hawa ni kama vile Daudi Kabaka, Fadhili Willliam, John Mwale na wengine. Baadaye katika miaka ya themanini na tisini, muziki wa bendi za muziki *Them Mushrooms* na *The Maroon Commandos* uliwekwa katika kategoria ya nyimbo zilizopendwa.

Kwa mujibu wa makala haya, muziki uliopendwa unarejelea nyimbo ambazo ziliimbwa kwa Kiswahili, zenye midundo ya taratibu, na ambazo zilikuwa maarufu katika miaka ya sitini, sabini, themanini na hata tisini. Nyimbo hizi zilipendwa na wasikilizaji wa wakati huo, na hata sasa zinapochezwa zinapendwa na wengi kwa sababu ya usanii uliotumika katika utungaji wa nyimbo hizo, mbali na mahadhi yaliyotokana na ala za muziki. Makala haya hayataangazia ala za muziki na midundo iliyotokana na ala hizo, bali yataegemea katika matumizi ya lugha pevu iliyokuwepo katika utungaji wa nyimbo hizo. Baadhi ya wasanii ambao kulingana na utafiti huu wanaweza kuwekwa katika kategoria ya muziki wa zilizopendwa ni pamoja na Cosmas Chidumule na bendi ya DDC Mlimani

Park, John Ngereza na bendi ya les Wanyika, Mbaraka Mwinshehe, Abel Kifoto wa Maroon Comandoes na wengine.

Ingawa kuna muziki unaofahamika kama 'zilizopendwa' ulioimbwa kwa lugha nyinginezo kama vile Kilingala, Kizulu, Kitswana na lugha nyinginezo za Kiafrika, katika makala haya, aina hiyo ya muziki haitajadiliwa bali tutazingatia muziki ulioimbwa kwa Kiswahili pekee.

Muziki wa kisasa

Ni muhimu ieleweke kuwa maisha yanaendelea kubadilika, kupitia uhusiano wa kijamii, kiuchumi, kitamaduni, kimazingira na hata kiteknolojia. Mabadiliko yanapoendelea kutokea, yanadhihirika kupitia nyimbo na tungo za muziki. Mabadiliko katika muziki hujitokeza katika aina ya muziki, ala zinazoandamana na muziki wenyewe na maudhui yanayozungumziwa katika muziki huo. Kwa muktadha huo, tunaweza kudai kwamba kila kizazi huwa na masuala yake ya 'kisasa', ukiwemo muziki. Mulongo (2012) anaeleza muziki wa kisasa kama uimbaji unaojumuisha masimulizi yakiandamana na midundo ya gitaa, piano, ngoma na ala zingine za muziki.

Okumu (1998) anadai kwamba muziki wa kisasa ni muziki unaotengenezwa studio, ukitumia vifaa vichache vya kisasa bila kuhitajika kundi kubwa la wapiga gitaa, ngoma na tarumbeta kuongozana hadi studio kurekodi kama bendi za zamani zilivyokuwa. Hata hivyo dai hili linaweza kuzua mjadala, kwani katika baadhi ya utunzi na uimbaji wa nyimbo za kisasa, bado kuna matumizi ya bendi na ala za muziki. Akishadidia hoja ya muziki wa kisasa kutotumia bendi. Ntarangwi (2007) anadai kwamba, "muziki wa kisasa ni ule ambao anaweza akakaa msanii mmoja na mwandalizi wake mmoja, basi, wakatengeneza albamu nzima kwa kutumia tarakilishi na vifaa vingine vya kisasa."

Kwa mujibu wa makala haya, muziki wa kisasa ni ule uliotungwa na wasanii walioko sasa na ambao umeibuka kuwa maarufu kwa wasikilizaji wa muziki katika kipindi cha sasa. Muziki huu unavuma na ni maarufu katika jamii, hususan miongoni mwa vijana. Aina hiyo ya muziki umetungwa kwa Kiswahili, Kiingereza na lugha nyinginezo. Hata hivyo, makala haya yamechagua muziki wa kikundi kimoja tu (*Sauti Sol*) kwa sababu kikundi hiki ni miongoni mwa vikundi ambavyo vimeibuka kupendwa na watu wengi, si tu nchini Kenya, bali pia katika bara la Afrika na hata nje. Muziki wa *Sauti Sol* umetungwa kwa mtindo wa mashairi yanayogusia masuala mbalimbali katika jamii ya sasa na huandamana na midundo ya ala za muziki zinazofanya muziki huo kuchezeka kwa urahisi na hivyo kupendwa na hadhira pana ya wasikilizaji wa muziki. Ingawa kuna bendi na waimbaji wengi ambao muziki wao unaweza kuingia katika kategoria ya muziki wa kisasa (kama vile *Diamond Platinumz*, *Kidum*, *Nameless*, *Nyashinski* na wengine) , katika makala haya tutachanganua tu muziki

wa kikundi kimoja. Azma ya makala haya ni kufanya ulinganisho kati ya muziki uliopendwa na muziki wa kisasa.

Umuhimu wa muziki katika jamii

Jamii nyingi ulimwenguni zimekuwa zikitumia muziki katika kujitambulisha na kuunda mitandao ambayo wanajamii wanaitumia katika kuandaa, kupokezana, na kusambaza habari muhimu. Kwa mfano kwa mujibu wa (Ntarangwi 2007), Waswahili hutumia muziki katika kukuza mahusiano miongoni mwa jamii yao. Njogu (2006), anadai kwamba katika tamaduni nyingi za Kiafrika, takriban kila sherehe na shughuli maishani kama vile kilimo, uvuvi, usasi, ususi, harusi na tanzia ziliambatana na nyimbo. Kila sherehe mathalani za unyago jandoni, akidi, kazi na kikoa, zilikuwa na ngoma zake spesheli.anaendelea kudai kwamba ushairi simulizi ndio zao la nyimbo nyingi zinazoimbwa na jamii za Kiafrika

Gachukia (2009) anazungumzia namna muziki wa kizazi kipya ulivyotumiwa na wasanii mbalimbali katika kuokoa taifa la Kenya dhidi ya ghasia za baada ya uchaguzi mwaka wa 2007. Anazidi kueleza kuwa wasanii walitunga nyimbo na mashairi kuhusu amani ili kuunganisha wananchi ambao walitawanyika kwa misingi ya kikabila. Maoni ya Adwar (2009) kuhusu muziki ni kwamba, muziki wa kizazi kipya na ukariri wa mashairi unaweza kuwasaidia vijana kukumbana na matatizo yanayohusu mabadiliko ya kimwili (adolesensi). Adwar (keshatajwa) anaendelea kudai kwamba sanaa ya muziki ndiyo inayoweza kuwapatia vijana fursa ya kukabiliana na matatizo ya kiujana. Anasisitiza haja ya kuhimiza uimbaji na ukariri wa mashairi miongoni mwa vijana ili kupanua na kukuza hulka nzuri. Kwa hivyo, kwa ukitazamwa kwa mapana, muziki una umuhimu mkubwa sana katika jamii.

Tamathali za Usemi

Kwa mujibu wa Ndungo (2006), tamathali za usemi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana zingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum iliyokusudiwa na mtunzi au mzungumzaji. Tamathali hutumika katika mazingira halisi ya mazungumzo ya wanajamii katika shughuli za kila siku za wanajamii hao. Zinapotumiwa, tamathali za usemi hulenga kutoa mawazo ya msemaji pamwe na kuibua hisia fulani katika msikilizaji. Wamitilla (2003) anafasili tamathali za usemi kama neno au kifungu ambacho kina maana iliyofichwa. Matumizi ya tamathali za usemi yamejitokeza sana sio tu katika riwaya au kazi za fasihi bali pia katika lugha ya kawaida. Kulingana na Kamusi Kuu ya Kiswahili (2017) tamathali ni usemi unaotumika kwa maana ambayo ni kinyume na maana ya kawaida ili kufunza jambo. Kamusi hiyo inaendelea kusema kwamba baadhi ya tamathali za usemi ni pamoja na sitiari, tasfida, tashbiha, tashihisi, tashtiti, balagha, tabaini na ritifaa. Mbali na tamathali za

usemi, makala haya yanachanganua pia methali na mafumbo yaliyotumika katika muziki wa uliopendwa na muziki wa kwani matumizi yake katika fasihi na hata mazungumzo ya kila siku ni dhihirisho la ujuzi wa lugha pevu.

Data na Uchanganuzi wake

Data iliyotumika katika makala haya ilitotoka na jumla ya nyimbo nne, Nyimbo mbili za kikundi cha *DDC Mlimani Park* (*Majirani huzima redio na Neema*) na nyimbo mbili za kikundi cha *Sauti Sol* (*Sura yako mzuri na Nerea*). Nyimbo zilizochaguliwa ni miongoni mwa nyimbo maarufu sana kutoka kwa kila kikundi. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa njia mbili. Njia ya kwanza ilikuwa ni kutafuta maneno ya nyimbo hizo kwenye mtandao kisha kuzisikiliza na kulinganisha maneno yaliyoandikwa na nyimbo zenyewe. Njia ya pili ilikuwa ni kusikiliza nyimbo na kisha kunakili maneno yake ambayo baadaye yalichanganuliwa. Maneno ya nyimbo za *Sauti Sol* ndiyo yalipatikana kwenye mitandao:(http://www.metrolyrics.com/sura-yako-mzuri-mama-lyrics-sauti-sol.html na https://www.musixmatch.com/lyrics/Sauti-Sol-feat-Amos-and-Josh/Nerea.) Maneno ya nyimbo za DDC Mlimani Park hayakupatikana kwenye mtandao na ilibidi mtafiti azisikilize na kisha kunakili maneno hayo. Baada ya kunakili nyimbo, nakala zilipatikana na ndizo zilitumika katika kudondoa tamathali za usemi, methali na mafumbo yaliyotumika katika nyimbo zenyewe. Kutokana na data hiyo, jedwali lifuatalo linaloonyesha ulinganisho wa matumizi ya vipengele tofauti vya lugha liliandaliwa.

Uliganisho wa vipengele vya lugha katika nyimbo za *DDC Mlimani Park* na za *Sauti Sol*

Kipengele cha Lugha	Sauti Sol	DDC Mlimani Park
Sitiari	2	5
Tashbihi	4	4
Misemo	3	4
Nahau	-	2
Methali	-	2
Mafumbo	-	2
Tafsida	-	4
Taniaba	1	-
Mdokezo	1	-
Mbalagha	-	1
Takriri	4	4
Kejeli	-	1
Jumla	**15**	**29**

Mapambo ya lugha katika nyimbo za DDC Mlimani

Jedwali hili linadhihirisha kuwa, kutokana na nyimbo mbili za *DDC Mlimani Park, Majirani huzima redio* na *Neema* kulikuwepo na jumla ya mapambo 29 tofauti ya lugha na idadi ya mapambo 15 katika nyimbo za *Sauti Sol, Nerea* na *Sura yako mzuri Mama* . Miongoni mwa mapambo yaliyotumika ni sitiari, tashbihi, misemo, tashhisi, methali, tafsida na mafumbo. Wingi wa matumizi ya mapambo ni dhihirisho la upevu wa lugha katika sanaa ya aina yoyote ile, (Wamitila 2003). Mbali na idadi kubwa ya matumizi ya mapambo ya lugha, mfuatano wake katika mishororo mbalimbali unadhihirisha matumizi ya lugha sanifu na pevu. Aidha, matumizi ya mapambo haya hufanya wimbo kuvutia, uwe na msisitizo na mnato mkubwa, kama mifano ifuatayo inavyoonyesha:

Mfano wa 1

Usipate taabu Neema (msemo)
Uliyoyafanya siyo mageni hapa duniani ee
Ikiwa ni kupendana mama (sitiari)
Wako waliopendana kama watoto mapacha (tashbihi)
Ikiwa ni mapenzi bibi (sitiari)
Wako waliopendana kama kumbikumbi (tashbihi)
Kumbikumbi ooo
Wanapendana sana
Hata wakati wa kutembea utawaona
Bibi mbele, bwana nyuma
Lakini sio ajabu hata pacha hutokea wakati
Wakakosa kuelewana aa (methali)
Tena kwa viapo oo Neema
Sembuse mimi na wewe (tashbihi)

(Dondoo kutoka ubeti wa kwanza wa wimbo *Neema* wa *DDC Mlimani Park*)

Mfano wa 2

Ninapata taabu moyoni mwangu mimi (msemo)
Kwa kweli
Nimekupenda wewe lakini hunijali mama (sitiari)
Tumekuwa sisi wawili
Kama sinema (tashbihi)
Hapa nyumbani kwetu kila siku kelele

Lakini kwa vile ee ee
Tunaishi hapa kwa wazazi wako
Mwenye sauti ni wewe (fumbo)
Naogopa fedheha mama oo mie
Naona aibu kweli mpenzi (msemo)
Hapa ni kwa wakwe zangu
Sisemi lolote, (fumbo)
Fanya upendavyo (fumbo)

(Dondoo kutoka kwa ubeti wa kwanza wa *Majirani huzima redio* wa *DDC Mlimani Park*)

Mifano hii ya beti za kwanza za nyimbo za *DDC mlimani Park* imesheheni jumla ya mapambo tofauti 15. Mapambo hayo ni pamoja na mafumbo, sitiari, misemo, tashbihi methali, miongoni mwa mapambo mengine. Hii ni idadi kubwa ya mapambo na inaweza kuchangia pakubwa katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa mtu anayezisikiliza nyimbo hizo mara kwa mara, hali hii hi tofauti na nyimbo za *Sauti Sol* ambazo zina idadi ndogo ya mapambo katika beti za kwanza za nyimbo mbili kama mifano ifuatayo inavyodhihirisha;

Mfano wa 3

Nimekuchagua wewe, Nikupende,
Mama... Sitaki mwingine,(sitiari)
Aushi usiniache... Usinitende, (msemo)
Mama... Usipende mwingine,
Moyo wangu ni mwepesi,(tashhisi)
Umenikalia chapati,(fumbo)
Nafanya vituko kama chizi,(tashbihi)
Kukupenda sitasizi,(Uchanganyaji msimbo pamwe na utohozi)
Moyo wangu ni mwepesi,
Umenikalia chapati,
Nafanya vituko kama chizi,
Kukupenda sitasizi

(kutoka ubeti wa kwanza wa kwanza wa wimbo *Sura yako Mzuri* wa *Sauti Sol*)

Mfano wa 4

Nakuomba Nerea, Usitoe Mimba Yangu We,(msemo)
Mungu Akileta Mtoto, Analeta Saa Ni Yake,(msemo)
Mlete Nitamlea, Usitoe Mimba Yangu We,
Mungu Akileta Mtoto, Analeta Saa Ni Yake,
(kutoka ubeti wa kwanza wa kwanza wa *Nerea* wa *Sauti Sol*)

Ubeti wa wimbo wa kwanza wa *Sura yako mzuri* una jumla ya tamathali 6 tofauti zilizotumika ilhali ubeti wa kwanza katika wimbo wa pili, *Nerea* una jumla ya tamathali mbili peke yake

Beti hizi mbili za mwanzo za nyimbo za *Sauti sol* zimesheheni jumla ya tamathali za usemi 8, idadi ambayo ni ya chini ikilinganishwa na ile ya nyimbo za *DDC Mlimani Park* ya 15.

Ulinganisho wa beti za kwanza umefanywa kwa vile mara nyingi mtu huupenda na kuendelea kuusikiliza wimbo fulani kutegemea utangulizi wake, hasa anapousikiliza kwa mara ya kwanza. Vile vile, endapo mtu atajifunza maneno ya wimbo wowote ule, mara nyingi hujifunza sehemu ya kwanza ya wimbo huo kwani ndiyo anayoisikia kwanza na hivyo ndiyo hunata akilini mwake.

Mbali na idadi ya tamathali za usemi na mapambo mengine lugha yaliyomo katika muziki wa *DDC Mlimani* na *Sauti Sol*, ulinganisho vilevile ulifanywa wa mtindo katika muziki huo. Utafiti huu uligundua kwamba ingawa ni desturi kwa nyimbo kuwa na kibwagizo ambacho hurudiwa mara kadhaa katika wimbo fulani, kuna mtindo wa uradidi uliodhihirika katika nyimbo za *Sauti Sol*. Mifano ya sehemu zifuatazo za nyimbo za Sauti Sol zinaweka wazi hoja hii.

Mfano wa 5

Maneno	**mshororo**
Huenda Akawa Obama, Atawale Amerika,	1
Huenda Akawa Lupita, Oscar Nazo Akashinda,	2
Huenda Akawa Wanyama, Acheze Soka Uingereza,	3
Huenda Akawa Kenyatta, Mwanzilishi wa Taifa,	4

Katika mfano huu, msanii wa wimbo huu amerudia maneno mawili ya kwanza ya ubeti huo. Sababu za uradidi zaweza kuwa msisitizo wa hoja inayojadiliwa, au pia huenda ikawa kwamba uradidi ulikusudiwa kutoa mpigo fulani na kuongezea mahadhi wa wimbo wenyewe. Hiki ni kipengee cha mtindo ambacho kilijitokeza katika muziki wa *Sauti Sol.* Aina nyingine ya uradidi ilitokea katika wimbo *Sura yako mzuri* ambapo kulikuwa na uradidi wa mshororo

mzima. Aina hii ya uradidi ilitokea katika sehemu ambayo ni kibwagizo cha wimbo, ambapo mbali na neno la kwanza baada ya kila mishororo miwili kuradidiwa, kuna mshorororo mzima uliorudiwa rudiwa. Mfano wa 6 unaonyesha hali hiyo.

Mfano wa 6

Maneno	**mshororo**
Sura yako mzuri mama, Aaaah	1
(Mzuri mama, mzuri mama, mzuri mama)	2
Na tabasamu lako maua, Aaaah,	3
(Mzuri mama, mzuri mama, mzuri mama)	4
Sura yako mzuri mama, Aaaah	5
(Mzuri mama, mzuri mama, mzuri mama)	6
Na tabasamu lako maua, Aaaah,	7
(Mzuri mama, mzuri mama, mzuri mama) [x2]	8
*Na **figure** yako kama ya chupa, Aaaah (uchanganyaji msimbo pamoja na tashbihi)*	9
(Mzuri mama, mzuri mama, mzuri mama)	10
Na tabasamu lako maua, Aaaah	11
(Mzuri mama, mzuri mama, mzuri mama	12

Katika mfano huu, neno *na* ambalo ndilo linaanza mishororo ya 3.7,9 na 11 limerudiwa. Aidha, maneno *Mzuri mama, mzuri mama, mzuri mama* yamerudiwa rudiwa baada ya kila mshororo, yaani katika mishororo ya 2, 4, 6, 8, 10 na 12, na hivyo kufanya sehemu hii kuchukua mtindo wa kibwagizo cha wimbo. Nilivyotangulia kusema, uradidi si aina ya tamadhali za usemi, lakini tumeujadili kwa vile ni kipengee cha matumizi ya lugha kilichojitokeza sana katika muziki wa *Sauti Sol.*

Makosa ya kisarufi katika nyimbo

Uchunguzi wa kina uligundua kwamba muziki wa *DDC Mlimani Park* haukuwa na makosa ya kisarufi, hata hivyo, muziki wa *Sauti Sol* ulipatikana na makosa machache ya kisarufi ambayo yanaweza kuwa na athari mbaya kwa ujifunzaji wa Kiswahili kupitia muziki. Makosa ambayo yaligunduliwa na ambayo yanaweza kuwa na athari hasi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili yanapatikana katika mishororo ifuatayo ambao ni sehemu ya kibwagizo cha wimbo *Sura yako mzuri mama* wa *Sauti Sol.* Sura ni mojawapo ya nomino zinazoingia katika ngeli ya N/N, na kwa hivyo inapotumika upatanisho wake wa kisarufi unatarajiwa kuwa N. Kwa mfano. Tungetarajia mshororo huo usome hivi:

Sura yako nzuri mama.

Katika kutumia sura mzuri badala ya sura nzuri, msanii amekiuka kanuni za kisarufi na akatumia *M* badala ya *N.* Uhuru huu wa kishairi unaruhusiwa kutumika na watunzi wa mashairi na hata nyimbo kwa sababu ya uhusiano kati ya vipera hivi viwili, hata hivyo kwa mtu anayejifundisha lugha kupitia kwa muziki huo, huenda asijue kwamba ni kosa kusema *sura mzuri* badala ya sura *nzuri.* Kwa hivyo, msikilizaji wa wimbo huo atajifunza sarufi mbovu kutokana na kusikilia wimbo huo.Kosa lingine la kisarufi liko katika mshororo ufuatao ambao unapatikana katika ubeti wa kwanza wa wimbo *Sura Yako mzuri wa sauti Sol*:

Juu moyo wangu ushakubali.

Katika mfano huo hapo juu, neno linalozua utata ni *juu.* Juu ni dhana inayotumiwa kimakosa kumaanisha *kwa vile* au *kwa sababu.* Katika Kiswahili sanifu, neno *juu* halina maana sawa na *kwa sababu.* Kwa hivyo, kutumia neno hilo kunadhihirisha uvunjaji wa sarufi ya Kiswahili.

Uchanganyaji Msimbo

Nyimbo za kikundi cha *Sauti Sol* zinadhihirisha matumizi mengine ya lugha kama vile uchanganyaji msimbo. Hebu turejelee mfano ufuatao:

Kukupenda sitasizi. (Katika ubeti wa kwanza wa wimbo *Sura Yako mzuri*)

Itabidi *nikumarry.* (Katika ubeti wa kwanza wa wimbo *Sura Yako mzuri*)

Analeta Saa Ni Yake. (Katika ubeti wa kwanza wa wimbo *Nerea)*

Neno *sitasizi* ni mfano wa uchanganyaji msimbo na vilevile utohozi katika neno hilo moja. Viambishi awali vya neno (*sita)* ni vya Kiswahili ilhali viambishi vya mwisho katika neno hilo (*sizi*) vimetoholewa kutoka kwa neno la Kiingereza ***cease*** lenye maana ya kuacha. Hali hii ya kuchanganya viambishi katika neno *sitasizi*, kunafanya mfano huo kuchukuliwa kama hali ya changanyaji msimbo. Hali ni tofauti kidogo katika matumizi ya neno *nikumarry.* Katika *ikumarry*, kuna uchanganyaji msimbo halisi kwa vile neno la Kiingereza *marry* limeunganishwa na viambishi vya Kiswahili *niku* katika kuunda neno *nikumarry*

Unganuzi wa mshororo *analeta saa ni yake,* unaonyesha kosa la kisarufi linalotokana na mpangilio wa maneno. Ingawa unaweza kuchukuliwa kama kuboronga sarufi, hali inayoruhusiwa katika utunzi wa mashairi, mshororo huo unazua utata. Wengi wa wasilikizaji wanaoufahamu wimbo huu hufasiri mshororo huo kama *sahani yake* na wala si *saa ni yake.*

Hitimisho

Makala haya yamelinganisha matumizi ya tamathali za usemi katika muziki wa zilizopendwa na muziki wa kisasa. Ulinganisho huo umehusu nyimbo mbili za bendi ya DDC Mlimani Park, ambayo nyimbo zake zilikuwa maarufu katika

miaka ya 1980 hadi 1990 na mbili za za Sauti Sol, kikundi cha uimbaji ambacho nyimbo zake ni maarufu sasa. Ulinganisho huo ulilenga kuonyesha ni muziki upi ulio na matumizi ya lugha pevu, na hivyo unaweza kutumika katika kufundishia lugha. Azma ya makala haya ilikuwa ni kuonyesha kwamba ingawa nyimbo ni kipera cha fasihi simulizi, zina uwezo mkubwa wa kutumika katika kufundishia vipengee vya sarufi. Ni muhimu kwa mkufunzi au mwalimu anayetaka kutumia nyimbo kuteua kwa makini aina za nyimbo ambazo anaweza kuzitumia, na wala asiongozwe na umaarufu wa wimbo au waimbaji waliouimba. Ninapendekeza kwamba, wasomi na wapenzi wa Kiswahili waweze kutumia muziki wa nyimbo zilizopendwa katika kufundishia vipengee anuwai vya lugha.

Marejeleo

Adwar, H A. (2009). "Managing Transition into Adolescence through performing Arts for active Learning, A Case of Elocution". A research paper presented at the 5th PPMC Symposium on Africa Music.

Gachukia, E. (2009). "The value of contemporary Kenyan Music in National cohesion and reconciliation. A research paper presented at the 5th PPMC Symposium on African Music"

Braza la Kiswahili la Kitaifa. (2014). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Nairobi, Longhorn publishers

Mindoti, K. W. (2014). The Compromised role of Kenya Indegenous Musical Expressions in Community Life. Katika *Kenya Journal of Musical Arts.* Vol 2. Pgs 19-29

Mulongo, M. O. (2012). Mchango wa muziki wa kizazi kipya katika ufundishaji wa ushairi wa Kiswahili kwenye shule za sekondari nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa.

Ndungo, C. (2006). "Matumizi ya Tamathali za Usemi katika lugha ya kisiasa" Katika, Njogu, K., Momanyi, C.,na Mathooko, M.(wh). *Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Nairobi, Twaweza Communication.

Ngugi, P.Y. (2000). "Nafasi ya Muziki Uliopendwa katika fasihi ya Kiswahili". Swahili Forum VII.145-152.

Njogu, K., Momanyi, C.,na Mathooko, M.(wh). (2006). *Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Nairobi Twaweza Communication.

Ntarangwi, M. (2007). "Music, Identity and Swahili Networks of Knowledge." Katika, Njogu, K. na Oluoch-Olunya *Cultural Production and Social Change in Kenya* : Nairobi, Kenya, E.A Twaweza Communications Ltd.

Nyandiba; C. (2014). *Ong'eng'o* for HIV/AIDS Education in Kisii Kenya. Katika . *Kenya Journal of Musical* Arts. Vol 2. Pgs 11-19.

Okumu, C. (1998). Development of Kenya popular Guitar Music.Study of Kiswahili songs. Unpublished MA thesis Kenyatta University. Nairobi

Shitandi, W. O. (2014). African Classical Drumming of *Ohangla* drum Ensemble of the Luo in Kenya: A Practical Guide. Katika *Kenya Journal of Musical Arts*. Vol 2. Pgs 107-128.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi, Focus Publications.